# Mkataba wa Kibali cha Kuingia na Uchaguzi kuhusu Ardhi

kati ya

**RP Global Holding Italy Srl**

na

**Halmashauri ya Kijiji cha Kilambo**

## Yaliyomo


1 Fasili na Ufafanuzi ..... 1
2 Kibali cha Kuingia ..... 4
3 Haki Kamili ..... 5
4 Kodi ya Kibali cha Kuingia ..... 5
5 Haki za Kampuni ..... 6
6 Haki endelevu ya kuingia na kutumia Ardhi ..... 6
7 Mipaka kuhusu Matumizi ya Ardhi ..... 7
8 Gharama na Matumizi ya Fedha ..... 7
9 Uchaguzi kuhusu Ardhi ..... 7
10 Viapo vya Halmashauri ya Kijiji [na] au Wamiliki wa Ardhi] ..... 8
11 Utekelezaji wa Uchaguzi ..... 8
12 Athari endelevu za Mkataba huu ..... 8
13 Uendelevu wa haki za kuingia katika eneo la ardhi ..... 8
14 Urithishaji ..... 8
15 Tathmini ya mtaalamu ..... 9
16 Ukiukaji wa Mkataba ..... 9
17 Masuala ya Jumla ..... 9
18 Taarifa na Anuani ..... 10
19 Lugha ..... 11
20 Usiri ..... 11
21 Sheria zinazohusika ..... 11
22 Mahakama ..... 11
23 Awamu za utekelezaji ..... 11
Jedwali 1: Eneo la Ardhi ..... 14
Jedwali 2: Muundo wa Taarifa ya Uchaguzi ..... 17
Jedwali 3: Hatua za kufuata baada ya kutolewa kwa Taarifa ya Uchaguzi ..... 18

## Mkataba wa Kibali cha Kuingia na Uchaguzi kuhusu Ardhi wa tarehe 2019

**Wahusika** **RP Global Holding Italy Srl**, kampuni binafsi iliyosajiliwa nchini Italia ikiwa na anuani ya usajili katika eneo la Viale della Stazione 7, 39100 Bolzano, Italia(**Kampuni**); na

**Halmashauri ya Kijiji cha Kilambo**, ni halmashauri ya kijiji iliyosajiliwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya IR/256 na iliyoopo katika kijiji cha Kilambo (**Halmashauri ya Kijiji**);

## Utangulizi

A Halmashauri ya Kijiji ina mamlaka na wajibu wa kusimamia eneo la ardhi ya Kijiji kama ilivyoelezwa katika Jedwali 1 (**Ardhi**).

B Wamiliki wa Ardhi ni wamiliki wa sehemu za Ardhi wanaotambulika na Halmashauri ya Kijiji kama walivyoorodheshwa chini ya Jedwali 2.

C Kampuni inataka kuingia Mkataba na Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi ili kupata kibali cha kuingia katika eneo la Ardhi kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi wa awali kuangalia uwezekano wa kujenga mradi wa umeme unaotumia nishati jadidifu (**Mradi**).

D Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wamekubaliana kwamba Halmashauri ya Kijiji itatekeleza huu Mkataba kwa niaba ya Wamiliki wa Ardhi.

E Baada ya kumaliza uchunguzi huu wa awali, Kampuni itapewa nafasi ya kufanya Uchaguzi kuhusu ardhi (kama inavyofafanuliwa hapa chini) kama inavyoonyeshwa kwenye Taarifa ya Uchaguzi (kama inavyofafanuliwa hapa chini). Kampuni inaridhia kuilipa mamlaka inayohusika Fidia kwa ajili ya zoezi la kufanya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria ya Tanzania.

F Kampuni hii ni ya kigeni, ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi inaweza kupewa ardhi kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

G Halmashauri ya Kijiji na au Wamiliki wa Ardhi wanakubali kuipatia kibali cha kuingia katika eneo la Ardhi Kampuni hii kwa madhumuni yaliyoelezwa kwenye Mkataba huu. Aidha, Halmashauri ya Kijiji na au Wamiliki wa Ardhi imekubali kuipatia Kampuni hii nafasi ya kufanya Uchaguzi (kama inavyofafanuliwa hapa chini) kwa mujibu wa vigezo vya Mkataba huu.

## Imeafikiwa

## 1 Fasili na Ufafanuzi

1.1 Katika Mkataba huu, isipokuwa kama muktadha utaonyesha vinginevyo:

(1) Kodi ya Kibali cha Kuingia kwenye Eneo inamaanisha kodi inayolipwa kwa Halmashauri ya Kijiji na au Wamiliki wa Ardhi wakati wa Kipindi cha Kibali cha Kuingia na kodi yoyote intakayolipwa kwa Kipindi cha Nyongeza;

(2) Kipindi cha Kibali cha Kuingia inamaanisha kipindi cha miaka 5 kuanzia Tarehe ya Kusaini au kusitisha mapema kabisa mkataba wakati wa kutolewa kwa Taarifa ya Uchaguzi;

(3) Makataba inamaanisha mkataba huu wa kibali cha kuingia na uchaguzi kuhusu ardhi;

(4) Msaidizi wa Kamishna wa Ardhi inamaanisha msaidizi wa Kamishna wa Ardhi;

(5) Siku ya Kazi inamaanisha siku yoyote ile kando ya Jumamosi, Jumapili au sikukuu ya kitaifa;

(6) Fidia inamaanisha fidia inayohusiana na Uchaguzi, kiasi kilichoafikiwa kulingana na thamani ya soko la ardhi na kulingana na Uchaguzi uliopendekezwa kwenye ripoti ya uthamanishaji wa ardhi iliyotolewa na mthamanishaji wa ardhi wa serikali;

(7) Kamishna wa Ardhi inamaanisha kamishna wa ardhi kama anavyoteuliwa chini ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;

(8) Halmashauri ya Wilaya inamaanisha halmashauri ya wilaya ya Waning'ombe iliyosajiliwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(9) Kipindi cha Nyongeza inamaanisha kipindi kisichozidi miaka 2 baada ya kuisha kwa Kipindi cha Kibali cha Kuingia katika Eneo la Ardhi bila kuhusisha utekelezaji wa Uchaguzi;

(10) Wamiliki wa Ardhi inaamanisha wamiliki wa arhi ambao ni watu wenye haki kwenye maeneo ya Ardhi amabyo iko chini ya Halmashauri ya Kijiji ndani ya wilaya ya Makambako na Mmiliki wa Ardhi inamaanisha, kama inavyostahili, mmoja wapo kama walivyoorodheshwa kwenye Jedwali 2;

(11) Waziri wa Ardhi inamaanisha waziri aliyeteuliwa na Rais ili kuongoza Wizara ya Ardhi;

(12) Wizara ya Ardhi inamaanisha wizara inayoshughulika na masuala ya ardhi;

(13) Uchaguzi inamaanisha haki zilizotolewa kwa Kampuni kwa mujibu wa kifungu cha 10 hapa chini, ambazo zinahusisha, bila ukomo wa uchaguzi kamili wa kuipata ardhi ambayo inafaa kwa biashara (kulingana na upimaji wa kufaa kwa Ardhi inayochunguzwa): (1) zimeachwa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kiweze kuuanzisha Mradi huu kulingana na sheria ya Tanzania (ambapo, Kituo cha Uwekezaji kitatoa hati isiyo asilia kwa jina la Kampuni); na (2) zimeelezwa kama barabara za kuingilia na kwa ajili ya kurahisisha miunganisho ya gridi, vyovyote vile itakavyokuwa zielezwe kwenye Taarifa ya Uchaguzi (imeelezwa hapa chini) katika kipengele cha vigezo na masharti kwenye mkataba wa manunuzi ya bidhaa;

(14) Taarifa ya Uchaguzi inamaanisha taarifa ya uchaguzi iliyopo kwenye muundo ulioelezwa katika 0 la Mkataba huu, ikifafanua maeneo ya Uchaguzi;

(15) Hesabu ya Malipo inamaanisha formula ya kuhesabu kiasi kwa kila Mmiliki wa Ardhi binafsi au Halmashauri ya Kijiji kiasi cha kodi watakacholipwa na Kampuni ,kwenye Kipindi cha Kibali Kuingia na Kipindi cha Nyongeza kama ifuatavyo:

5/6 ya kodi iliyolipwa kati ya Kipindi cha Kibali Kuingia au Kipindi cha Nyongeza itaenda kwa Wamiliki Ardhi; na

1/6 ya kodi iliyolipwa kati ya Kipindi cha Kibali Kuingia au Kipindi cha Nyongeza itaenda kwa Wamiliki wa Ardhi;

(16) Hati ya Uwakilishi inamaanisha hati ya uwakilishi iliyosainiwa na kila Mmiliki wa Ardhi akiteua Halmashauri ya Kijiji kama mwakilishi wao kwa ajili ya huu Mkataba kama ilivyoelezwa ndani ya Jedwali 3;

(17) Rais inamaanisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(18) Msajili wa Hati Miliki inamaanisha msajili aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334;

(19) Tarehe ya Kusaini inamaanisha tarehe ya saini ya mwisho kwenye Mkataba huu;

(20) Kipindi cha Mpito inamaanisha kipindi ambacho masharti ya 0 yanatumika;

(21) Kijiji inamaanisha kijiji cha Kilambo kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya), Sura ya 287 na kipo katika kata ya Luhota, Wilaya ya Iringa Vijijini, Mkoa wa Iringa, Tanzania; na

(22) Baraza la Kijiji inamaanisha baraza la kijiji kinachohusika.

1.2 Urejeaji wowote katika Mkataba huu kwenye:

(1) Kifungu ni, kutegemeana na ukinzani uliotokea, rejea ya kifungu cha Mkataba huu;

(2) Sheria inamaanisha sheria yoyote ikiwa ni pamoja na sheria za nchi, sheria zinatotungwa na bunge, katiba, amri, hukumu, mkataba, kanuni, maagizo au sheria ndogo au hatua yoyote ya serikali, serikali ya mtaa, au maagizo yanayowekwa na mamlaka ya kutunga sheria au kanuni au mahakama ikiwa na mamlaka ya kisheria; na

(3) mtu inamaanisha mtu halisi au mtu wa kisheria, kampuni, shirika, serikali, nchi, wakala, au chombo, asasi, mfuko (aliye au asiye na nafsi huru kisheria)

1.3 Pale neno au kifungu cha maneno kinapopewa maana maalum, aina nyingine za maneno na maneno ya kisarufi au kifungu cha maneno chenye maana sawa.

1.4 Vichwa vya habari haviongozi wala kuathiri tafsiri ya Mkataba huu.

1.5 Kama sehemu ya fasili zilizotolewa inatoa haki, au inamtwika majukumu Mhusika yeyote, itachukuliwa kwa uzito kama jambo la muhimu katika Mkataba huu.

1.6 Isipokuwa kama muktadha unaonyesha vinginevyo, maneno yanayoonyesha jinsia yanahusisha jinsia; rejea ya mtu halisi inahusisha mtu wa kisheria, umoja inahusisha hata wingi, na wingi inahusisha umoja.

1.7 Idadi yoyote ya siku zilizoelezwa katika Mkataba huu inaondoa siku ya kwanza na inahusisha siku ya mwisho; na kitendo chochote au tangazo lolote litakuwa na maana litakapofanywa au kutolewa katika siku ya mwisho.

1.8 Isipokuwa kama muktadha utaonyesha vinginevyo, kama siku ya malipo ya kiasi chochote au utekelezaji wa jukumu lolote unaangukia katika siku ambayo siyo Siku ya Kazi, siku hiyo itahamishiwa katika siku nyingine ya kazi inayofuatia hapo.

1.9 Maneno "pamoja na" na "na hasa" hayana ukomo.

1.10 Rejea yoyote kwenye sheria ni kwa sheria hiyo kama ilivyo katika Tarehe ya Kusaini, kama itakavyofanyiwa marekebisho au kubadilishwa kwa nyakati tofauti.

1.11 Rejea yoyote kwenye waraka wowote au sheria inahusisha waraka huo kama ilivyopitishwa, ulivyofanyiwa maboresho, marekebisho au kubadilishwa kwa nyakati tofauti.

1.12 Rejea kwa Mhusika ni pamoja na warithi halali na wasimamizi wake.

1.13 Muda wa siku ni ule muda wa saa za Dar es Salaam.

1.14 Kanuni ya kutafsiri Mkataba kwamba, pale ambapo kuna utata, mkataba unatakiwa kutafsiriwa mbele ya Mhusika aliyeandaa mkataba, haitumiki hapa.

1.15 Kusitishwa kwa Mkataba huu hakuathiri vile vipengele ambavyo kwa uwazi vinaonyesha kwamba vitatekelezwa hata baada ya Mkataba kusitishwa, au ambavyo kwa busara ya kawaida vinatakiwa kuendelea hata baadaa ya kusitishwa kwa Mkataba.

## 2 Wahusika

2.1 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wamekubaliana kwamba Halmashauri ya Kijiji itatekeleza huu Mkataba kwa niaba ya Wamiliki wa Ardhi. Kila Mmiliki wa Ardhi atatoa Hati ya Uwakilishi kwa Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya huu Mkataba.

2.2 Halmashauri ya Kijiji itawawakilish Wamiliki wa Ardhi kwenye maswala yote yanayohusiana na utelekelezaji na uendelezaji wa huu Mkataba. Kazi ya Halmashauri ya Kijiji kama mwakilishi itajumlisha na sio tu kusaini Mkataba, kusajili hati zinazohusiana na huu Mkataba na kupokea fedha kwa niaba ya Wamiliki wa Ardhi kama ilivyoelezwa kwenye kipengele 5.

## 3 Kibali cha Kuingia

3.1 Mkataba huu utaanza rasmi katika Tarehe ya Kusaini na utadumu kwa Kipindi chote cha Kibali cha Kuingia, Kipindi cha Nyongeza na Kipindi cha Mpito isipokuwa kama utasitishwa mapema zaidi.

3.2 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wanaipatia Kampuni haki kamili ya kuingia katika eneo la Ardhi na kuendesha shughuli kwa mujibu wa kifungu 12 cha Mkataba huu katika Kipindi chote cha Kibali cha Kuingia katika Eneo la Ardhi kulingana na idhini iliyotolewa na Baraza la Kijiji, Halmashauri ya Kijiji na Halmashauri ya Wilaya.

3.3 Pale ambapo Uchaguzi kuhusu Ardhi haukufanyika wakati wa kuisha kwa Kipindi cha Kibali cha Kuingia katika eneo, Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wanaipatia Kampuni haki kamili ya kuingia katika eneo la Ardhi wakati wa Kipindi cha Nyongeza kwa vigezo na masharti kama yaliyotolewa katika Kipindi cha Kibali cha Kuingia katika eneo.

3.4 Kipindi cha Nyongeza kitaanza mara moja baada ya Kipindi cha Kibali cha Kuingia katika eneo la Ardhi kuisha na kuendelea katika Kipindi chote cha Nyongeza isipokuwa kama Kampuni itaipatia Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi taarifa ya maandishi ya kusitisha Mkataba huu.

3.5 Baada ya kuisha kwa Kipindi cha Nyongeza na pale ambapo hakuna Uchaguzi uliofanyika, Mkataba huu utasitishwa.

3.6 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wanaipatia Kampuni haki kamili ya kuingia katika eneo la Ardhi wakati wote wa Kipindi cha Mpito.

## 4 Haki Kamili

4.1 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi haitampatia mtu mwingine haki yoyote katika au kwenye Ardhi, ambaye anaendana au haendani na haki zinazotolewa kwa Kampuni kwa mujibu wa Mkataba huu.

4.2 Katika mazingira ambapo Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wanapokea maombi ya kibali cha kuingia kwenye ardhi kwa mtu mwingine ili kufanya uchunguzi au utafiti ambao unaweza kukinzana kabisa na/au kuvuruga haki zinazotolewa kwa Kampuni, Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi itatakiwa kuijulisha mara moja Kampuni.

4.3 Halmashauri ya Kijiji, Wamiliki wa Ardhi, Kampuni na mhusika mwingine watakubaliana kuhusu haki zozote za kuingia katika eneo la Ardhi ambazo atapewa mtu mwingine na ambazo hazitaathiri Mradi katika Kipindi chote cha Kibali cha Kuingia, Kipindi cha Nyongeza na Kipindi cha Mpito na maendeleo yoyote ya Mradi mara tu Uchaguzi kuhusu Ardhi utakapofanyika.

## 5 Kodi ya Kibali cha Kuingia

5.1 Kampuni itailipa Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi Kodi ya Kibali cha Kuingia kwa Kipindi cha Kibali cha Kuingia na Kipindi cha Nyongeza.

5.2 Kampuni itailipa Halmashauri ya Kijiji kiasi TZS 6,000,000.00 kama kodi maalum kwa ajili ya matumizi ya Ardhi wakati wa Kipindi cha cha Kibali cha Kuingia.

5.3 Kampuni itailipa Halmashauri ya Kijiji kiasi TZS 3,000,000.00 kama kodi maalum kwa ajili ya matumizi ya Ardhi wakati wa Kipindi cha Nyongeza.

5.4 Halmashauri ya Kijiji itapokea Kodi ya Kibali cha Kuingia iliyoplipwa kwa mujibu wa kipengele 5 na kuigawanya kwa Wamiliki wa Ardhi kwa kutumia Hesabu ya Malipo.

5.5 Kodi ya Kibali cha Kuingia italipwa siku 14 baada ya Tarehe ya Kusaini pale ambapo Halmashauri itatoa taarifa ya maandishi kwa Kampuni ikiwa na maelezo ya benki kwa ajili ya malipo.

5.6 Kodi ya Kibali cha Kuingia itagawanywa kwa Wamiliki wa Ardhi binafsi na Halmashauri ya Kijiji ndani ya siku 7 kutoka siku malipo yalifanywa na Kampuni amayo pia itatoa uthibitisho wa maandishi wa malipo kwa Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi.

5.7 Kodi zozozte zinazopaswa kulipwa wakati wa Kipindi cha Kibali cha Kuingia katika eneo la Ardhi na Kipindi cha Nyongeza yatakuwa ni malipo ya mara moja tu kutoka katika Kampuni hii kwenda kwa Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi.

5.8 Hakutakuwa na kodi yoyote ya kulipa katika Kipindi cha Mpito.

## 6 Haki za Kampuni

6.1 Wakati wa Kipindi cha Kibali cha Kuingia, Kipindi cha Nyongeza na Kipindi cha Mpito, Kampuni itakuwa na haki kamili kufanya shughuli zake kwenye Ardhi kwa ajili ya maendeleo wa Mradi, ikiwamo:

(1) kusimikavifaa vya kuchunguza kuhusu upepo, jua, na hali ya hewakatika eneo la Ardhi;

(2) kutunza na kufanyia matengenezo vifaa pamoja na kuchukua taarifa kutoka kwenye vifaa hivyo;

(3) kuandaa barabara za kuingia kwenye eneo la vifaa;

(4) kufanya utafiti au uchunguzi, ikiwamo utafiti wa masuala ya kiufundi, mazingira, utafiti na tathmini za kijiolojia;

(5) kujenga uzio wa kulinda vifaa;

(6) kuweka alama za kutambulisha vifaa hivyo kuwa ni mali ya Kampuni;

(7) kuwa na utulivu wa mazingira wakati wote;

(8) haki ya kuingia katika eneo la Ardhi kupitia kwenye ardhi ya majirani ndani ya Kijiji; na

(9) kupata maji na kuchimba kisima, ambacho kinaweza kuhitajika wakati wa ujenzi wa Mradi.

6.2 Kama itagundulika kwamba Ardhi haifai kwa Mradi, Kampuni itakuwa na haki ya kusitisha Mkataba huu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa muda usiopungua mwezi mmoja kwenda katika Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi. Taarifa hiyo inaweza kutolewa wakati wowote katika Kipindi cha Kibali cha Kuingia na Kipindi cha Nyongeza.

6.3 Vifaa vyovyote vya kuchunguza kuhusu upepo, jua, ndege na popo, pamoja na uzio uliowekwa na Kampuni vitaendelea kuwa mali ya Kampuni na vinaweza kuondolewa na Kampuni mwishoni mwa Kipindi cha Kibali cha Kuingia au Kipindi cha Nyongeza.

## 7 Haki endelevu ya kuingia na kutumia Ardhi

7.1 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wataendelea kufanya shughuli zao kwenye Ardhi kwa kuzingatia masharti ya kifungu 13.

7.2 Shughuli zozote zinazoendeshwa na Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi hazipaswi:

(1) kuzuia uchunguzi wa awali katika eneo;

(2) kuharibu vifaa vya Kampuni au Ardhi ya eneo la Mradi; au

(3) kukwamisha kwa namna yoyote uchunguzi wa awali unaofanywa na Kampuni.

## 8 Mipaka kuhusu Matumizi ya Ardhi

8.1 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi watahakikisha kwamba:

(1) hakuna jengo wala miundombinu yoyote kama vile minara ya mawasiliano, nyumba, nk. zinajengwa bila kupata kwanza ukubali wa maandishi kutoka kwa Kampuni, ambapo inaweza kuachwa katika uamuzi wa Kampuni;

(2) shughuli zozote za kilimo zinazofanyika kwenye Ardhi hiyo zitaruhusiwa kuendelea kufanyika wakati wa Kipindi chote cha Kibali cha Kuingia na zitasimama tu kwa baadhi ya maeneo kutegemeana na zoezi la utekelezaji wa Uchaguzi; na

(3) watapaswa kutoa taarifa ya Mkataba huu, haki ya kuingia, uchaguzi wa kupata ardhi, na haki kamili kwa mnunuzi, mkodishaji, mpangaji, mhamiaji au mtu yeyote mwenye au anayetaka kuwa na au kupata maslahi kwenye Ardhi.

## 9 Gharama na Matumizi ya Fedha

9.1 Kampuni itailipa Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi gharama na matumizi ya fedha zote zilizotumika katika majadiliano, maandalizi, utekelezaji na utendaji wa Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi kuhusiana na Mradi huu kama tu shughuli hizo ziliidhinishwa awali na Kampuni.

## 10 Uchaguzi kuhusu Ardhi

10.1 Katika kipindi chaKibali cha Kuingia na Kipindi cha Nyongeza, Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wanaipatia Kampuni haki kamili ya kutekeleza Uchaguzi kuhusu Ardhi kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Uchaguzi kwa madhumuni ya kujenga Mradi wa uwekezaji.

10.2 Ardhi inayohusika katika Uchaguzi itajumuisha ardhi yote iliyopatikana kwa ajili ya kujenga mtambo ya sola, barabara za kuingilia kwenye eneo, maeneo ya miunganisho ya gridi na majengo pamoja na miundombinu yoyote inayosaidia kuwezesha ujenzi na uendeshaji wa mitambo ya upepo.

10.3 Kampuni ni mwekezaji wa nje, ambaye kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi anaweza kupewa ardhi kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Kwa mantiki hiyo, na kwa kuzingatia zoezi la Uchaguzi, ardhi ya ujenzi wa Mradi kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Uchaguzi, itatolewa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania na ardhi ya kuifikia ardhi iliyotolewa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kuwezesha namna ya kuingia kwenye eneo linalohusika, itatolewa kama barabara ya kuingilia na kwa ajili ya kurahisisha miunganisho ya gridi na itaonyeshwa kwenye mchoro wa matumizi ya ardhi ya kijiji.

10.4 Uchaguzi utatekelezwa kwa kuzingatia kanuni zilizoelezwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Kijiji, Sura ya 114, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 na sheria na kanuni nyingine pamoja na malipo ya Fidia.

10.5 Utekelezaji wa Uchaguzi utafanyika tu kwenye ardhi iliyoelezwa kwenye Taarifa ya Uchaguzi. Uchaguzi huu lazima uidhinishwe kwa mujibu wa mchakato uliobainishwa kwenye 0.

## 11 Viapo vya Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi

11.1 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wanasimama, inaahidi na kuapa kwa Kampuni kwamba:

(1) Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi wana umiliki halali wa Ardhi na haina wala haidaiwi na mtu yeyote na haina ubia na mtu mwingine;

(2) Mkataba huu ni halali na unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania;

(3) kwamba kodi ya mwaka inayopaswa kulipwa kwa serikali kuhusiana na Ardhi hii imeshalipwa hadi kufikia tarehe ya kusaini Mkataba huu; na

(4) ikitokea mtu mwingine ametokea mwenye madai halali kwenye Mali hii ambayo yalikuwepo hata kabla ya kusainiwa kwa Mkataba huu, Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi itapaswa mara moja kushauriana na Kampuni kuhusu uhalali wa madai hayo.

## 12 Utekelezaji wa Uchaguzi

12.1 Taarifa ya utekelezaji wa Uchaguzi itatolewa wakati wowote na mara kwa mara wakati wote wa Kipindi cha Kibali cha Kuingia na Kipindi cha Nyongeza kwa kuangalia kama ni sehemu yote au sehemu ndogo ya Ardhi na kutoa Taarifa ya Uchaguzi kwenye Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi. Taarifa ya Uchaguzi itabainisha ardhi ambayo inahusika.

12.2 Kufuatia zoezi la Uchaguzi na kabla Kampuni haijapewa hati isiyo ya asili na Kituo cha Uwekezaji Tanzania na utoaji wa mchoro wa matumizi ya ardhi kuonyesha barabara za kuingilia, na kwa kuzingatia masharti ya sheria zinazohusika, Kampuni itakuwa na haki zote za kuingia katika eneo la ardhi wakati wote wa Kipindi cha Kibali cha Kuingia na Kipindi cha Nyongeza kama ilivyoelezwa kwenye Kipindi cha Mpito.

## 13 Athari endelevu za Mkataba huu

Mkataba huu unatumika na unatekelezwa kwa manufaa ya warithi wa wahusika wote, wasimamizi na wawakilishi wao wote (kwa kadiri itakavyowezekana).

## 14 Uendelevu wa haki za kuingia katika eneo la ardhi

Haki zozote zilizotelewa wakati wa Kipindi cha Kibali cha Kuingia, Kipindi cha Nyongeza na Kipindi cha Mpito za kutumia barabara na kujenga miunganisho ya gridi pamoja na eneo la ardhi kwa ajili ya matumizi ya kawaidia ya Kijiji na Kampuni, zitaendelea kuwepo hata baada ya kusitishwa au kuisha kwa Mkataba huu na zitakuwa na nguvu na athari ileile.

## 15 Urithishaji

Kampuni ina haki ya kurithisha, kuuza au kutoa au hata kutoa maslahi yote au sehemu ya maslahi au manufaa au haki au wajibu ulioelezwa kwenye Mkataba huu wakati wowote, ikiwamo haki za Uchaguzi zilizoelezwa katika kifungu cha 10.

## 16 Tathmini ya mtaalamu

16.1 Mgogoro wowote au tofauti katika masuala ya Fidia itawasilishwa kwa maafisa wa Halmashauri ya Wilaya ambao wanashughulika na masuala ya ardhi. Gharama zozote zitakazotozwa na maafisa hao, zitagawiwa kwa namna sawa kwa Wahusika wote ambao kwa pamoja na kwa uelewa wa pamoja watachukua jukumu la kulipa.

16.2 Afisa huyo anapaswa kuwa anafanya kazi kama mtaalamu na siyo msuluhishi na uamuzi wake kuhusu kiasi cha Fidia utakuwa wa mwisho na utawahusu Wahusika wote.

## 17 Ukiukaji wa Mkataba

17.1 Ikiwa Mhusika yeyote (Mhusika anayekiuka Mkataba) atakiuka kipengele chochote cha Mkataba huu huyo Mhusika mwingine (Mhusika aliyeathirika) anaweza kumpatia Mhusika anayekiuka Mkataba taarifa ya kimaandishi ya siku 30 au muda mrefu zaidi ya huo kama atakavyoonyesha Mhusika aliyeathirika katika taarifa yake, kushughulikia huku kuvunjwa kwa mkataba. Kama Mhusika anayevunja Mkataba anashindwa kutimiza hili, Mhusika Anayeathirika anaweza:

(1) kudai malipo ya mara moja na/au kumtaka Mhusika anayekiuka Mkataba kutekeleza majukumu yake ambayo Mhusika anayevunja Mkataba anawajibika kuyatekeleza; au

(2) kufuta Mkataba huu baada ya kupeleka taarifa ya maandishi kwa Mhusika anayevunja Mkataba kuhusu ukiukaji wa Mkataba huo una athari kubwa,

katika lolote lile kati ya hayo mawili, bila kuathiri haki ya Mhusika anayeathirika kudai fidia au kutaka haki zingine zozote ambazo Mhusika Anayeathirika anaweza kuwa nazo kutokana na Mkataba huu au kwenye sheria.

17.2 Ufutaji wowote wa Mkataba huu utakaofanywa na Mhusika Aliyeathirika utatambulika baada ya kupokea taarifa ya Mhusika Anayevunja Mkataba (katika mazingira ya ukiukaji wa mkataba usiona na msamaha) au tarehe ya kukiuka mkataba (kwa mujibu wa mazingira yaliyoelezwa katika kifungu cha 17.1(2)).

Mhusika yeyote anaweza kufuta Mkataba huu kwa taarifa ya maandishi ili mradi jukumu ambalo Mhusika aliyeathirika amekwama kulifanya ni jukumu la muhimu katika Mkataba huu

17.3 Ufutaji wowote wa Mkataba haufuti madai yoyote ambayo Mhusika yeyote anaweza kuwa nayo kutokana na kukiukwa kwa masharti na vigezo vya Mkataba huu kulikofanywa na Mhusika mwingine na atayawasilisha kabla ya tarehe ya kufuta Mkataba.

## 18 Masuala ya Jumla

18.1 Mkataba huu ndio makubaliano yote kati ya Wahusika kuhusiana na jambo hili.

18.2 Hakuna nyongeza au mabadiliko au kufutwa kwa Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na kifungu hiki, ambayo haina athari isipokuwa kama itafanyika kwa maandishi na kusainiwa na Wahusika wote.

18.3 Hakuna uzembe uliofanywa na Mhusika mmoja kwa Mwingine, au kushindwa kutekeleza masharti ya Mkataba huu, ambao utasamehewa wala kutumika kujenga mazingira ya kusitisha Mkataba huu.

18.4 Wahusika wanakubaliana kufanya jambo lolote linalowezekana kwa uwezo wao wote kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Mkataba huu.

18.5 Jambo lolote ambalo ni kosa la kisheria au lisilotabirika katika Mkataba huu linaweza kuachwa na vifungu vinavyobaki vya mkataba huu vitaendelea katika utekelezaji.

## 19 Taarifa na Anuani

19.1 Taarifa

Taarifa yoyote, ukubali au mawasiliano mengine yoyote kuhusiana na Mkataba huu (**Taarifa**) itatolewa kwa maandishi na kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.

19.2 Anuani

(1) Kila Mhusika anapaswa kuchagua anuani ya makazi, namba ya faksi na/au anuani ya barua pepe kulingana na jina lake hapa chini kama anuani ambayo Taarifa yoyote itakuwa ikitumwa kwa anuani hiyo.

(a) Mhusika 1:

Anuani ya Makazi: Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Jengo la Utawala, Malimbe-Nyamagana

P.O Box 307, Mwanza

Anuani ya barua pepe: j.pendezza@rp-global.com

Inakusudiwa ielekezwe kwa: Msanidi wa Mradi; na

(b) Mhusika 2:

Anuani ya Makazi: Kilambo village

P.O. Box 2455, Iringa

Anuani ya barua pepe: Haihusiki

Inakusudiwa ielekezwe kwa: Afisa Mtendaji wa Kijiji

(2) Mhusika yeyote anaweza kwa kutoa Taarifa kwa Mhusika mwingine kubadilisha anuani yake na/au mtu yeyote, kama yupo, ambaye Taarifa yake inatakiwa kuonekana katika kifungu cha 19.2(1).

19.3 Kupokelewa kwa taarifa

(1) Tarifa yoyote itaanza kutekelezwa baada ya kupokelewana Mhusika(au katika muda mwingine wa baadaye ulioelezwa kwenyeTaarifa hiyo) na, isipokuwa kama imethibitishwa vinginevyo, taarifa hiyo itachukuliwa kwamba imepokelewa:

(a) katika siku ya kukabidhiwa, kama itakabidhiwa kwa mkono kwa Mhusika kwa anuani ya makazi kwa mujibu wa kifungu cha 19.2. Kama Taarifa hiyo itakabidhiwa katika Siku ambayo siyo ya Kazi, au baada ya saa za kazi za Siku ya Kazi, Taarifa hiyo itachukuliwa kuwa ilipokelewa katika siku ya kazi baada ya tarehe ya kukabidhiwa; na

(b) katika Siku ya kwanza ya Kazi baada ya tarehe ya kutumwa, kama imetumwa kwa barua pepe kupitia anuani ya barua pepe ya mpokeaji iliyotolewa katika kifungu cha19.2.

(2) Isipokuwa kama kuna jambo lolote kinyume na Mkataba huu, Taarifa ambayo imepokelewa na Mhusika inatambulika hata kama haikutumwa, kukabidhiwa au kutumwa kwa anuani yake kwa mujibu wa kifungu cha 19.2.

19.4 Huduma za michakato ya kisheria

(1) Kila Mhusika atachagua anuani ya yake ya makazi ambayo imewekwa katika kifungu cha 19.2(1)kama anwani yake na nyaraka zingine za mambo ya kisheria kuhusiana na Mkataba huu yanaweza kupelekwa hapo.

(2) Mhusika yeyote anaweza kwa kutoa Taarifa kwa Mhusika kubadilisha anuani yakeambapo nyaraka za mambo ya kisheria na nyaraka nyingine kuhusiana na Mkataba huu zinaweza kupelekwa katika anuani nyingine ya makazi nchini Tanzania.

## 20 Lugha

Mkataba huu na marekebisho yake utafanyika kwenye nakala nne halisi zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza na nakala nne halisi zilizoandikwa lugha ya Kiswahili. Taarifa zote zitakazokuwa zikiandikwa, zitaandikwa kwa lugha ya Kiingereza na zitaelekezwa kwenye anuani rasmi ya watia saini walioidhinishwa na Wahusika kama inayoonyeshwa katika kifungu cha 19.2(1). Kama kutatokea tofauti au kupishana kati ya nakala ya Kiingereza na ile ya Kiswahili, nakala ya Kiingereza itatumika.

## 21 Usiri

21.1 Halmashauri ya Kijiji, Wamiliki wa Ardhi na Kampuni wanakubaliana kwamba haki na wajibu wa Halmashauri ya Kijiji, Wamiliki wa Ardhi na Kampuni kwa mujibu wa Mkataba huu, na masharti pamoja na malipo yaliyoelezwa kwenye Mkataba huu ni siri kabisa.

21.2 Halmashauri ya Kijiji na Wamiliki wa Ardhi haitatoa tangazo kwenye vyombo vya habari au tangazo lolote kuhusiana na au kuhusu Mkataba huu bila kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kampuni hii.

## 22 Sheria zinazohusika

Mkataba huu unatekelezwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

## 23 Mahakama

Wahusika bila masharti wanakubali kujisalimisha katika Mahakama yenye mamlaka husika Tanzania kwa madai yoyote, madai au migogoro yoyote ambayo inaweza kujitokeza kutokea au kuhusiana na Mkataba huu.

## 24 Awamu za utekelezaji

Mkataba huu utatekelezwa kwa awamu, na kila awamu ikajitegemea na zote kwa pamoja zikaunda Mkataba huu.

**Mbele ya MASHAHIDI HAWA**, Halmashauri ya Kijiji na Kampuni wanatia saini na kukubaliana na masharti na vigezo vya Mkataba huu kwa tarehe iliyotajwa awali hapo juu.

**IMETIWA SAINI** na **Kampuni**
kwa niaba ya

| | | | |
|---|---|---|---|
| Saini: | | Saini: | |
| Jina: | JACOPO PENDEZZA | Jina: | JUSTIN VICTOR MWANDA. |
| Cheo: | PROJECT DEVELOPER | Cheo: | CONSULTANT |

**IMETIWA SANINI NA Halmashauri ya Kijiji**
kwa niaba ya

| | | | |
|---|---|---|---|
| Saini: | | Saini: | |
| Jina: | ALDO OSWARD MFEPUNDA | Jina: | OLIVO R' UTENGA |
| Cheo: | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji | Cheo: | Afisa Mtendaji wa Kijiji, Kijiji cha Kilambo |

MWENYEKITI KIJIJI CHA KILAMBO IRINGA

AFISA MTENDAJI KIJIJI KILAMBO IRINGA

**Mkataba huu umeshuhudiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini**

Saini:.........................

Jina:.....FAUSTA MYINGA.....

Cheo: Wakili/~~Hakimu~~ Ag

Anuani:.........../18.........

DISTRICT LEGAL OFFICER IRINGA DISTRICT COUNCIL

Jedwali 1: Eneo la Ardhi


Iringa Solar Plant - Kilambo village
- 323 hectar / 798 acres
- Coordinate System: Decimal Degrees
Date: 02.05.2019
Author: Jacopo Pendezza
For:
RP Global Holding Italy Srl
Legend
project site
Y/X coordinates of the boundaries
Y -7.828882° X 35.771274°
Y -7.829386° X 35.765829°
Y -7.830640° X 35.770445°
Y -7.831083° X 35.767931°
Y -7.835143° X 35.759207°
Y -7.836796° X 35.761122°
Y -7.836139° X 35.787275°
Y -7.839490° X 35.785323°
Y -7.840121° X 35.767435°
Y -7.843049° X 35.782470°
Y -7.843494° X 35.771131°
Y -7.844796° X 35.779936°
Y -7.845448° X -7.845448°
Google Earth
1 km

**Jedwali 2: Orodha ya Wamiliki wa Ardhi na ukumbwa wa maeneo yaliyoshikiliwa**

| | | |
|---|---|---|
| | HUSSENI Jafari mfilinge | 5.5 |
| =) | ANJELA . C . MSWETE. | 1 3/4 |
| =) | EDDY EDWARD MYOVELA | |
| 4 =). | GEORGE . p. myovela. | 9.0 |
| 5 =) | CECIL . L . HAULE. | 11.0 |
| 6 =) | ALDO OSWARD MAPUNDA. | 3.5 |
| (7) | SHABANY JUSTINO | 12.0 |
| (8) | MITRAS MYOVELA | 4.0 |
| (9) | GODFREY MYOVELA | 1.0 |
| 10 = | CASTORY . C . MDOTA. | 3.5 |
| 11) =) | DISIMA MYINGE | 6.0 |
| 12 =) | KASTANSIA MWINGILA | 6.5 |
| 13 =) | KASIMU . J . SANGA | 10 |
| 14 =) | AIGBA SALUMU MBUTA | 3.1 |
| 15 =) | LEAH F. NGOGO | 2.0 |
| 16. | BONIFACE . G . NZENGELE | 17.0 |
| 17. | MILTONI . G . MYOVELA. | 35.0 |
| 18. | NKUPAKA MBONGELA | 2.0 |
| 19 | ANDERSON FRANK MATIVILA | 2.0 |
| 20 | DONATUS GOLACHUMA KINDOLE. | 31.0 |
| 21 = | GODFRY LAURENT MBIMBI | 1.0 |
| 22 =) | ANNA . Z . MWINGILE | 6.0 |
| 23 =) | JAMES . C . MYOVELA | 6.0 |
| 24 =) | BRUNO MATHESHED MBUTA | 3.5 |
| 25 =) | ALBERTHO . G . KAWAGANISE. | 1.0 |
| 26 =) | NATSON MATHESHED MBUTA. | 1.0 |
| 27 =) | ENTER . C . MSWETE. | 1.75 |
| 28 =) | AGUSTINO . P . MYOVELA. | 20.0 |
| 29 =) | PERAJA . R . UTENGA. | 11.0 |
| 29 =) | RICHARDY . 1 . MWANILWA | 40.0 |
| 30 =) | ANASTASIA S KIKOVE. | 10.0 |
| 31 =) | OSCAR PETER MBUTA. | 15.0 |

Mmmmt.

Otkrrith

/KH

| | | |
|---|---|---|
| 3- | MARCHERO PASCAL KAWAGANISE | 6.0 |
| 33- | ANJELO MAHESHE MBUTA | 11.0 |
| 34- | ELIZABETH PANGAYENA CHAHE | 15.0 |
| 35- | ANJERO .T. GEKA | 1.0 |
| 36- | SHERIDA IGNAS MKINGULE | 30.0 |
| 37- | JAPHET NYOMOLELO | 2.0 |
| 38- | BEST .T. KINDOLE | 17.0 |
| 39- | ANDREAS .P. CHAHE | 3.0 |
| 40- | BENITHO .Y. KAWAGANISE | 16.0 |
| 41- | HAJI .T. KINDOLE | 10.0 |
| 42- | EDMUND .S. TENYWA. | 28.0 |
| 43- | RAULENT .J. SAMILA | 1.0 |
| 44- | PASCAL NYOMOLELO | 3.5 |
| 45- | DICKSON .P. MBUTA. | 4.0 |
| 46- | AMON PETER MBUTA. | 3.0 |
| 47- | EMILYO .J. SAMILA | 1.25 |
| 48- | TIMOTHEO .J. KINDOLE | |
| 49- | EVA ERNESTO BALAMA. | 2.0 |
| 50- | VARENTINO WIRBAT TENYWA | 12.5 |
| 51- | ATILIO ROMANUS MHAPA. | 20.0 |
| 52- | EDGAR .A. NINDI | 3.5 |
| 53- | GUDLUCK THOMAS KISANGA. | 3.5 |
| 54- | SYLVESTER .B. MWANGAMILA | 2.0 |
| 55- | DANIEL ROMANUS MBUTA | 2.0 |
| 56- | OSCAR .PETER MBUTA | 15.0 |
| 57 | AGATHA MOHAMED MLULA | 48.0 |

KH

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | BERNADETHA. G. MHINGILE ✓ | — | 6.0 |
| 9- | ANDRU MBUTA | — | 4.0 |
| 60- | DOMINICK MHULILA | — | 3.0 |
| 61 | ZUNGUMZA MUHINGILE | — | 2.0 |
| 62 | MATHIAS - S. LUHWAGO | — | 12.0 |
| 63 | YOSEPHINA. M. NYINGE | — | 2.0 |
| 64 | EDINA MLULA. | — | 1.5 |
| 65 | ATILIO DONATUS KINDOLE | — | 3.0 |
| 66 | EMERITA . Z. MUHINGILE | — | 2.0 |
| 68 | LOMANA MUHINGILE. | — | 1.5 |
| 69 | AYUBU YAHAYA LUWINGO | — | 13.0 |
| 70. | ALBERTHO SAID MWIWULA. | — | 2.0 |
| 71 | WILLIAM. P. MGONGOLWA | — | |
| 72. | MAGDALENA. MKINGULE | — | |
| 73. | FELISTA CHOGISASI MSWETE | — | 1.0 |

Jedwali 3: Nakala za Hati za Uwakilishi

## Jedwali 4: Muundo wa Taarifa ya Uchaguzi

| | | |
|---|---|---|
| Tarehe | : | **[•]** |
| Kwenda kwa | : | [**Halmashauri ya Kijiji]** |
| Nk | : | **[Halmashauri ya Wilaya]** |
| Kutoka kwa | : | **[Upepo Tanzania Limited]** |

**[TAARIFA YA KUTEKELEZA UCHAGUZI] AU [TAARIFA YA KUTOTEKELEZA UCHAGUZI]**

Tunarejelea Mkataba wa Kibali cha Kuingua na Uchaguzi kuhusu Ardhi (Mkataba wa Uchaguzi) wa tarehe [•] 2019 uliofanyika kati yetu na ninyi, kuhusiana na Uchaguzi.

Vigezo vilivyoelezwe kwenye Mkataba wa Uchaguzi vina tafsiri ile ile hata hapa.

Hapa tunakupatia taarifa kwamba sisi **[**tunataka **kutekeleza Uchaguzi] [hatutekelezi Uchaguzi]** kwa mujibu wa vigezo na masharti ya Mkataba wa Uchaguzi [kwa maeneo yaliyoteuliwa kama inavyoonyeshwa kwenye kiambatisho cha Taarifa hii ya Uchaguzi]:

Wako mtiifu

________________________

Jina:

Cheo:

Kwa ajili ya na kwa niaba ya[•]

## Jedwali 5: Hatua za kufuata baada ya kutolewa kwa Taarifa ya Uchaguzi

1. Kampuni itaamua kutekeleza Uchaguzi wa kununua ardhi na kuwajulisha Wahusika wa Mkataba huu kwa maandishi na kwa muundo ulioelezwa katika 0.

2. Kampuni itaomba ardhi hiyo kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania, ikieleza mahali ardhi ilipo na aina ya Mradi unaokusudiwa kutekelezwa.

3. Kampuni itawasiliana na Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Kijiji kuhusu utekelezaji wa Uchaguzi.

4. Vikao vya Halmashauri ya Kijiji na Baraza la Kijiji vitakaa ili kujadili suala hili na kuwasilisha kumbukumbu zake kwenye Halmashauri ya Wilaya.

5. Wahusika wote watakaa kujadili na kuamua kuhusu uandaaji wa mpango wa kutumia ardhi ya kijiji, uthamanishaji wa ardhi kutegemeana na Uchaguzi ulliofanyika, malipo ya fidia na Tathmini ya Athari kwenye Mazingira (Environmental Impact Assessment-**EIA**).

6. Halmashauri ya Wilaya itaidhinisha maamuzi ya Kijiji na kuyatuma kwenda Wizara ya Ardhi.

7. Waziri wa Ardhi atawasilisha majumuisho yote kwa Rais ili yaidhinishwe.

8. Baada ya Rais kuidhinisha, fomu ya ardhi ya kijiji namba 8 itaandaliwa na kuchapwa kwenye gazeti la Serikali ikielezwa kwamba baada ya siku 90, ardhi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania itahamishwa kutoka katika umiliki wa kijiji na kwenda kwenye matumizi ya jumla. Baada ya hapo, kama hakutakuwa na pingamizi, ardhi ya Kituo cha Uwekezaji itahamishiwa kwenye matumizi ya jumla.

9. Msaidizi wa Kamishna wa Ardhi ataandaa fomu ya ardhi namba 1 na kuichapa kwenye gazeti la Serikali na nakala zake zitapeleka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania na maafisa wengine wa ardhi walioidhinishwa ili kusaini.

10. Fomu ya Ardhi Na. 1 itatangazwa kwenye gazeti na Msaidizi wa Kamishna wa Ardhi kupitia sehemu ya waraka wa serikali.

11. Kamati ya upangaji ardhi ya taifa itaitishwa ili kujadili na kuidhinisha ardhi itolewe kwa Kampuni hii.

12. Baada ya kuidhinishwa na kamati ya upangaji ardhi ya taifa, Kampuni, pale ambapo ni muhimu, itaomba marekebisho ya hati yake ili kuingiza hati ya umiliki wa ardhi iliyotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

13. Baadae, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kitamwomba Kamishna wa Ardhi atoe ankara ya kodi inayopaswa kulipwa na Kampuni (ushuru wa forodha, kodi ya pango na kodi ya wateja wakubwa) ili kuweza kuandaa hati miliki ya ardhi kwa jina la Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Aidha, Kampuni itatakiwa kukilipa Kituo cha Uwekezaji Tanzania 10% ya gharama za uwezeshaji.

14. Kampuni hii itawasilisha kwa Kamishna wa Ardhi uthibitisho wa malipo ya kodi hiyo.

15. Waziri wa Ardhi ataandaa na kutoa fomu ya kukiri kupokea malipo ili ikasainiwe na Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Baada ya kusainiwa, fomu hiyo itarudishwa kwa Msaidizi wa Kamishna wa Ardhi.

16 Msaidizi wa Kamishna wa Ardhi ataandaa rasimu ya hati miliki kwa jina la Kituo cha Uwekezaji Tanzania na kuipeleka kwenye Kituo hicho kwa ajili ya kusainiwa.

17 Msaidizi wa Kamishna wa Ardhi atasaini hati miliki na kuiwasilisha kwa Msajili wa Hati Miliki kwa ajili ya usajili.

18 Baada ya kukamilisha hati miliki, hati itatolewa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

19 Kituo cha Uwekezaji Tanzania kitaandaa haki miliki isiyo ya asili na maombi ya kukodisha ardhi, na wahusika wote, Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Kampuni, watasaini waraka huo.

20 Kituo cha Uwekezaji Tanzania kitawasilisha haki miliki isiyo ya asili na maombi ya kukodisha ardhi kwa Msajili wa Haki Miliki.

21 Kituo cha Uwekezaji Tanzania kitachukua haki miliki isiyo ya asili na maombi ya kukodisha ardhi kutoka kwa Msajili/Msajili Msaidizi wa Hati Miliki na nakala moja itatolewa kwa Waandaaji wa Mradi/Wawekezaji.